**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKONDARI TEULE**

S.L.P 248
MBEYA.
06/12/2020

KUMB.NA.MoVET/S.2095/JOINING/2021

JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………………………..
S.L.P …………………
**MBEYA.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TEULE WILAYA YA MBEYA MWAKA 2020**

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 shule ya sekondari **TEULE**
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/01/2020** ndani ya siku tano

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**


**2.1 Sare ya shule**

a) Sare ya shule hii ni suruali moja ya **kijani** na moja **nyeusi**, mashati mawili meupe ya mikono mifupi kwa wavulana na sketi moja kijani na moja nyeusi (iwe ndefu inayofika usawa wa soksi), blauzi mbili nyeupe mikono mifupi kwa wasichana. Mshono wa kawaida na nguo za heshima
b) Sare ya michezo kwa shule hii ni T-shirt moja **dark blue**(utaipata shuleni) na bukta moja kwa wavulana na wasichana T-shirt moja **dark blue** (utaipata shuleni) na sketi ya michezo pamoja na track suit nyeusi kwa wote wavulana na wasichana.
c) Sweta rangi ya kijani
d) Viatu vyeusi vya Ngozi vya kufunga na Kamba kisigino kifupi kwa wasichana na wavulana
e) Soksi **nyeupe** kwa wasichana na soksi **nyeusi** kwa wavulana.

**2.2 VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

Madaftari kumi na moja (counter book 2 quire) mkebe, rula na kalamu zote wino na risasi

**KARIBU SANA**



**……………….**
**E.A.SAFARI**
**MKUU WA SHULE**
**0764507495**

**NB: SIKU YA KURIPOTI SHULENI UFIKE UMEVAA TRUCK SUIT SIYO UNIFOFORM ZINGATIA HILI**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

3.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine ni muhimu.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare za shule wakati wote.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

### 3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.


1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji bangi
5. Makossa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau bendera ya taifa
9. Kuoa au kolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

## 4.0 Mambo mengine muhimu

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa serikali, fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shule.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia , kanuni, kulipa michango na maelezo mengine yatakayotolewa na shule

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATKA SHULE HII**



**……………….**
**E.A.SAFARI**
**MKUU WA SHULE**
**0764507495**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKONDARI TEULE**
**FOMU YA AHADI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

## A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………………………………. Msichana/mvulana
Ninakubali kuingia kidato cha ……. Shule ya sekondari Teule kama mwanafunzi wa kutwa. Tarehe …………….. nitafika shuleni bila kukosa au kuchelewa.
Nitatii sheria zote za shule na nitaishi Maisha mazuri na a mfano. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidi katika masomo na kazi na kujitegemea, sitakuwa mtoro shuleni.
Sahihi ya mwanafunzi …………………………………….. tarehe …………………

## B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

1. Mimi ………………………………………………………. Ninakubali mtoto wangu ……………………………………………………….. asome katika shule ya sekondari Teule kuanzia tarehe …………………… ninaamini kuwa elimu ni urithi wa mtoto na mwanga wa Maisha.

2. Ninaahidi kumpatia vitu anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyoagizwa katika barua yako.

3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria zote za shule na kuishi katika maisha mazuri na mfano kwa wenzake. Nitamhimiza asome kwa bidii katika masomo yake na kazi za kujitegemea. Nitamhimiza asiwe mtoro.

4. Ninakubali kuwa mtoto wangu amukubali kusoma katika shule ya sekondari Teule kama mwanafunzi wa kutwa na ataendelea hivyo hadi kumaliza kidato cha nne (iv). Mimi stamhamisha kwenda shule nyingine pasipo sababu

5. Namba ya simu mzazi/mlezi ………………………………….

6. Sahihi mzazi/mlezi ………………………………… Tarehe …………………..

7. Pia ikumbukwe wazazi walipata kibali toka kwa mkuu wa mkoa cha kuchangia pesa za weekly test **SHS.20,000** na **LIMU MOJA KWA MWAKA** hivyo mzazi utambue huo ni mkakati wa kuinua taaluma shuleni na hizo pesa anapokea **MWENYEKITI WA WAZAZI MZEE PETRO PAMOJA NA LIMU MOJA A4** (walimu hatupokei michango hivyo usimpe mwalimu mchango wowote)

## C. KWA MATUIZI YA OFISI

Mwanafunzi ………………………………………………………………. Amepokelewa
Tarehe……………………………………………
SAHIHI ……………………………..

NB: Nafasi za hosteli kwa wasichana zipo, utaratibu wa kujiunga na hosteli utatolewa kwa anayetaka awasiliane na uongozi wa shule